



## BODI YA BIMA YA AMANA

### KATIKA SHAURI LA EFATHA BANK LTD (CHINI YA UFILISI) NA

### KATIKA SHAURI LA SHERIA YA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA, 2006 (THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, 2006)

#### TAARIFA KWA UMMA

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba **EFATHA BANK LTD** imewekwa chini ya ufilisi na Benki Kuu ya Tanzania kuanzia tarehe 4 Januari, 2018. Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 41 (a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, 2006 (The Banking and Financial Institutions Act, 2006) Benki Kuu ya Tanzania imeiteua Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board –DIB) taasisi ilioanzishwa chini ya kifungu cha 37 (1) cha Sheria tajwa kuwa Mfilisi wa Benki hiyo.

Kufuatia uteuzi huo, Mfilisi wa **EFATHA BANK LTD**, Bodi ya Bima ya Amana (DIB), inatoa taarifa kwa wadai na wadaiwa wote wa benki hiyo kama ifuatavyo;

- (a) Wadaiwa wote wa **EFATHA BANK LTD** na mtu yoyote anayeshikilia mali ya Benki hiyo ikiwa ni pamoja na kumbukumbu au nyaraka na vifaa vyovyyote vya ofisi anataarifiwa kwamba ali pe madeni hayo, arudishe kumbukumbu/nyaraka na mali za benki hiyo kwa Mfilisi (DIB) kuititia anuani iliyotajwa hapo chini kabla ya siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2018. Wale watakaokaidi taarifa hii watachukuliwa kwamba wanashikilia mali hizo kinyume cha sheria kuanzia siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2018. .
- (b) Vile vile, wadai wote ambaio sio wenye amana (Depositors) wa **EFATHA BANK LTD** (chini ya ufilisi) wanataarifiwa kuleta madai yao yakiwa na uthibitisho kamili kwa Mfilisi kwa kutumia anuani iliyotolewa hapo chini kabla ya siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2018. .

#### Mkurugenzi

**Bodi ya Bima ya Amana**

**Jengo la Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania**

**2 Mtaa wa Mirambo**

**Ghorofa ya 7, Mnara wa Kaskazini**

**11884 DAR ES SALAAM**

**Email: DIB-INFO@bot.go.tz**

**TEL: +255 22 223 5390**

**Fax: +255 22 223 4200**

**IMETOLEWA TAREHE 17 MACHI, 2018**